

HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA

SHULE YA SEKONDARI LAINI,
S.L.P 469,
ITILIMA.

Tarehe.....

Simu Na. 0624227527 au 0755156235

KWA

SHULE YA MSINGI.....

ITILIMA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LAINI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Laini. “**HONGERA SANA**”

2. MAHARI SHULE ILIPO

Shule ipo kijiji cha **Laini ‘B’** kata ya **Sagata** Tarafa ya **Bumera** wilaya ya **Itilima**.

3. KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021**
Uchelewaji pasipo sababu za msingi hautavumiliwa na **sheria kali** zitachukuliwa dhidi yako.

4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(A) SARE ZA SHULE

i. Wavulana

- Suruali mbilimoja **zambarau** iliyoiva na nyingine ya **light blue** iliyoiva (vitambaa vimeambatanishwa)
- **Tai** mbili za rangi ya suruali
- Shati mbili **nyeupe za tetro** mikono mifupi aina ya **tomato**
- Viatu **veyeusi** jozi mbili vya ngozi vyenye visigino vifupi na viwe na kamba na **siyo raba nyeusi**
- Soksi fupi jozi mbili rangi **nyeupe**
- Viatu vya michezo (**raba**) rangi nyeupe
- Sweta rangi ya **kijani** kwa ajili ya baridi
- **Trucksuit** rangi ya zambarau kwa ajili ya michezo
- Fulana (T-shirt) za **kora** rangi **nyekundu** kwa ajili ya shughuli za jioni

ii. Wasichana

- Sketi mbili moja **zambarau** iliyoiva na nyingine **light blue** iliyoiva (vitambaa vimeambatanishwa)
- **Tai** mbili za rangi ya sketi
- Shati mbili **nyeupe za tetro** mikono mifupi aina ya **tomato**
- Viatu **veyeusi** jozi mbili vya **ngozi** vyenye visigino vifupi na viwe na kamba na **siyo raba nyeusi**
- **Soksi** ndefu aina ya **stocking** jozi mbili rangi **nyeupe**
- Viatu vya michezo (**raba**) rangi nyeupe
- Sweta rangi ya **kijani** kwa ajili ya baridi
- **Trucksuit** rangi ya zambarau kwa ajili ya michezo
- Fulana (T-shirt) za **kora** rangi **nyekundu** kwa ajili ya shughuli za jioni

(B) VIPIMO VYA USHONAJI

Wavulana

- Suruali iwe na rinda 2 na ruksi 6
- Mkanda nchi moja na nusu ($1\frac{1}{2}$)
- Paja nchi 23
- Chini nchi 18
- Mifuko 3
- Suruali iwe na **turnup**
- **N. B. Fundi anaposhona azingatie vipimo kwa kuzigatiam umbo la mhusika mwenyewe**

Wasichana

- Marinda ya kati
- Mkanda nchi moja na nusu ($1\frac{1}{2}$)
- Sketi ifike kwenye **kifundo cha miguu**

5. MAHITAJI MENGINE

- Mwanafunzi aje na daftari counter book quire two (2) au three (3) zisizopungua kumi na moja
- Begi zuri kwa ajili ya kubebeta daftari (**mifuko ya Bob haitakiwi**)
- Karamu za wino na risasi
- Mkebe wa hesabu (mathematical set)
- Aje na kamusi ya kiingereza kwa Kiswahili
- Mwanafunzi awe na saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda

6. MASOMO YAFUNDISHWAYO

- Masomo yafundishwayo ni kumi (10) ambayo ni:-
Chemistry, Biology, physics, Basic mathematics, Agriculture, History, Geography, Kiswahili, Civics na English
- **Masomo yote hufundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili.**
- **Lugha ya mawasiliano ni kiingereza tu.**

7. MENGINEYO

- Sheria, kanuni na taratibu za shule zimeambatanishwa
- Mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi mnatakiwa kuzisoma na kuzilewa pamoja na kuzisaini.
- **Pindi unapo ripoti njoo na sheria hizo zikiwa zimesainiwa**

8. MUHIMU

- Sare ambazo hazitazingatia vigezo/vipimo hazitaruhusiwa hivyo mzazi/mlezi uwe makini katika ushonaji
- **Wakati wa kuripoti uje na mzazi pamoja na vifaa vyote ulivyoagizwakwa ajili ya ukaguzi**

Kauli mbiu ya shule ni:-“Nullification of Ignorance to the society”

Nakutakia maandalizi mema,

ELIAH A. MWASUMBI
(Mkuu wa shule)

SHULE YA SEKONDARI LAINI

SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

(A) SHERIA ZA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuepuka kabisa makosa yafuatayo:-

Haya yanaweza kusababisha afukuzwe shule kwa mujibu wa sheria ya wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundii:-

- (i) Wizi wa aina yoyote
- (ii) Ugomvi, lugha chafu, kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzako au mtumishi
- (iii) Udanganyifu katika mitihani ya aina yeyote ile
- (iv) Kujaribu, kusababisha na kuongoza na kushiriki kugoma kwa wanafunzi au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni
- (v) Ubakaji/ulawiti/ushoga/usagaji
- (vi) Uasherati pamoja na kupatikana kwa vifaa vya aina hiyo
- (vii) Ulevi wa aina yeyote
- (viii) Uvutaji wa sigara, Bangi na madawa ya kulevyia pamoja na uuzaaji
- (ix) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule/umma na ya watu wengine
- (x) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
- (xi) Kutoa mimba, kushiriki au kushawishi kutoa mimba ndani na nje ya shule
- (xii) Kukataa adhabu halali kwa makusudi
- (xiii) Kudharau bendera na wimbo wa Taifa /Viongozi wa serikali picha za viongozi wa Taifa, nembo ya taifa na fedha za Taifa
- (xiv) Kuoa au kuolewa
- (xv) Kutoonekana shuleni miezi mitatu utafukuzwa na Bodi ya shule

(B) KANUNI MUHIMU ZA SHULE

- (i) Mwanafunzi anapaswa kuwa mtii, mwenye adabu na mnyenyeketu nyakati zote na popote. Zaidi ya yote awe na nidhamu ya hali ya juu
- (ii) Mwanafunzi akiwa nje ya darasa asimame na kusalimia kwa heshima na adabu kwa walimu na wageni wote watakaotembelea shule.
- (iii) Marufuku kuonyesha au kujaribu mahusiano ya kimapenzi, wanafunzi wote ni watoto wa familia moja.
- (iv) Nilazima kila mwanafunzi kuvalaa sare sahihi za shule wakati wote na nyakati za shule.
- (v) Marufuku kwa mwanafunzi kuonekana kwenye vilabu vya pombe, baa, kumbi za starehe, kumbi za mpira na majumba ya kulala wageni (guest house) pamoja na sehemu zenye michezo ya bahati nasibu mfano bonanza na pooltable
- (vi) Ni marufuku kuvalaa heleni, pete, kofia, kufuga nywele ndefu na ndevu, kupaka rangi kucha za vidole na midomo pamoja na kutochomekea shati.
- (vii) Ni marufuku kuongea lugha zisizo rasmi shuleni mfano kisuma. Kiingereza ni lugha ya pekee ya mawasiliano wakati wote shuleni.
- (viii) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi au laini ya simu shuleni na nje ya shule.
- (ix) Ni lazima kila mwanafunzi aoneshe bidii kubwa katika masomo darasani, pamoja na mitihani ya mara kwa mara inayotolewa ndani na walimu.
- (x) Ni marufuku kuletwa au kuchukuliwa na usafiri wa gari, wala daladala za baisedeli na pikipiki hapa shuleni. Wanafunzi wote wanapaswa kuja shuleni na kurudi nyumbani kwa miguu au baisedeli za nyumbani ili kujenga ukakamavu.
- (xi) Ni marufuku kuonekana mitaani baada ya 12:30 jioni ukionekana hatua kali zitachukuliwa dhidi yako
- (xii) Nimarufuku kutumia vipodozi, kubadilisha ngozi na kuweka nywele dawa
- (xiii) Mwanafunzi unatakiwa kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- (xiv) Mwanafunzi unatakiwa kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (xv) Mwanafunzi unatakiwa kutunza mali ya umma/shule
- (xvi) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (xvii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuri ndani na nje ya shule ni muhimu
- (xviii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea nyumba za walimu isipokuwa kwa kibali maalum
- (xix) Mwanafunzi unatakiwa uheshimu kengele
- (xx) Kila mwanafunzi ahakikishe anazuia na kukamata mifugo kuingia eneo la shule

❖ **Kwa mengine yote ambayo huna uhakika nayo, uliza kwa walimu au viongozi wateule.**

Jina la mzazi/mlezi..... sahihi.....tarehe.....

Jina la mwanafunzi..... sahihi.....tarehe.....